# Makubaliano ya Mshirika wa Ufikishaji[1]

Makubaliano haya ya Mshirika wa Ufikishaji wa Grubhub ("Makubaliano") yametengenezwa na kukubaliwa kati ya Grubhub Holdings Inc. ("Grubhub"), kampuni ya Delaware, iliyo na makao makuu ya biashara kwenye anwani ya 111 W. Washington St., Suite 2100, Chicago, IL 60602 na wewe, mtaalamu huru wa ufikishaji aliyetia sahihi hapa chini ("Mshirika wa Ufikishaji" au "Wewe"). Grubhub na Mshirika wa Ufikishaji wanaweza kurejelewa hapa ndani, kila mmoja kama "Mhusika" na pamoja kama "Wahusika." Makubaliano haya yataanza kutumika tarehe ambayo yanakubaliwa bila kujali kama wewe unastahiki, au hata utawahi stahiki, kutekeleza Shughuli yoyote (kama ilivyobainishwa hapa chini).

**Tafadhali pitia Makubaliano haya kwa makini, pamoja na sehemu ya "Usuluhishaji wa Pamoja" iliobainishwa hapa chini katika Sehemu ya 13, kwani itakuhitaji kusuluhisha migogoro na Grubhub, bila kujali wakati inaibuka au kuwasilishwa, kupitia mchakato binafsi wa usuluhishaji, isipokuwa ujiondoe kihalali kwenye mchakato wa usuluhishaji, kama ilivyobainishwa hapa chini. Unatambua na kukubali kwamba wewe na Grubhub kila mmoja wenu anaondoa haki ya kufanya kesi yenye waamuzi. Pia unaondoa haki yako ya kushiriki kama mlalamikaji au mhusika katika kesi yoyote ya pamoja au kesi ya uwakilishi dhidi ya Grubhub, iwe imesubirishwa au itaandikishwa katika siku zijazo. Unatambulisha moja kwa moja kwamba umesoma na umeelewa, na unakubali kufungwa na sheria na masharti haya yote ya Makubaliano haya na umechukuwa muda kuzingatia madhara ya uamuzi huu muhimu. Kwa kutumia Programu ya Driver (kama ilivyobainishwa hapa chini), unakubali kufungwa na Makubaliano haya, na pia Sheria za Matumizi za Mshirika wa Ufikishaji wa Grubhub, Sera ya Faragha ya Mshirika wa Ufikishaji wa Grubhub, Sheria za Matumizi za Grubhub, pamoja na sera na miongozo mingine yoyote inayoweza kuchapishwa mara kwa mara.**

Jedwali la Yaliyomo


Maelezo……1
Sheria na Masharti……2
1. Madhumuni……2
2. Uwakilisho na Uhakikisho wa Mshirika wa Ufikishaji……2
3. Matumizi ya Programu ya Driver……4
4. Huduma za Ufikishaji……4
5. Ada za Huduma na Ankara……7
6. Uhusiano wa Wahusika……7
7. Wanakandarasi Wadogo……8
8. Uondoaji Lawama……8
9. Kipimo cha Dhima……9
10. Mchakato wa Kisheria Unaoathiri Akaunti ya Mshirika wa Ufikishaji……9
11. Faragha na Vikwazo vya Kutumia Maelezo ya Kibinafsi……9
12. Kipindi; Ubatilishaji……11
13. Usuluhishaji wa Pamoja……12
14. Uondoaji Haki ya Kesi ya Pamoja……15
15. Marekebisho……16
16. Mambo Mengine……16


## Maelezo

Grubhub ni kampuni ya oda za chakula za mtandaoni na tamba ambayo inawapatanisha wateja na mikahawa ya ndani na ya ufikishaji na/au biashara nyingine (kwa pamoja, "Muuzaji/Wauzaji") kupitia tovuti yake na programu husiani za simu (kwa pamoja, "Mfumo"). Grubhub si kampuni ya ufikishaji au msafirishaji wa kawaida. Lakini,

[1] Ilisasishwa Desemba 4, 2024

kupitia mfumo wake uliowezeshwa mtandaoni, Grubhub inawezesha kuweka oda ya chakula, ikijumuisha kuchukuliwa na wateja wenyewe na ufikishaji na Wauzaji kwa misingi ya inapoagizwa. Pia Grubhub inawezesha ufikishaji wa chakula kutoka kwa Wauzaji fulani ambao hawana chaguo la ufikishaji kwa kuwapatanisha Wauzaji na wateja wa ndani pamoja na Washirika huru wa Ufikishaji, ambao wanafikisha chakula kutoka kwa Wauzaji hao hadi kwa wateja wanaoweka oda kupitia Mfumo ("Huduma za Ufikishaji").

Mshirika wa Ufikishaji ni msafirishaji huru, mwenye leseni na/au huduma za ufikishaji, na ana nia ya kuingia katika Makubaliano haya ili kupata nafasi ya kufikisha oda zilizowekwa na wateja kupitia Mfumo ili kupata ada za huduma ("Ada za Huduma") zitakazokubalianwa kati ya Wahusika. Mshirika wa Ufikishaji anamiliki na/au kudhibiti vifaa na wafanyikazi wote wanaohitajika kutekeleza Huduma za Ufikishaji kulingana na sheria husika. Mshirika wa Ufikishaji anaelewa na kukubali moja kwa moja kwamba Wewe si mwajiriwa wa Grubhub wala Muuzaji yeyote, biashara nyingine, au mtu anayetumia Mfumo wa Grubhub na kwamba Wewe unatekeleza Huduma za Ufikishaji kwa niaba yako mwenyewe na biashara yako, na si kwa niaba ya Grubhub. Mshirika wa Ufikishaji anaelewa kwamba: (i) Wewe uko huru kujadili mapato yako, miongoni mwa mambo mengine, kwa kukubali au kukataa Huduma za Ufikishaji zilizowasilishwa kupitia Mfumo wa Grubhub, na unaweza kufanya maamuzi hayo ili kugeuza nafasi Yako ikawa faida; na (ii) Wewe una haki binafsi ya kudhibiti namna ambavyo Huduma za Ufikishaji zinatekelezwa na njia kwa ambayo Huduma hizo za Ufikishaji zinakamilishwa kulingana na sheria.

Tukizingatia ahadi za pamoja zilizowekwa hapa ndani, Wahusika wanakubaliana na sheria na masharti yaliyobainishwa hapa ndani.

1. <u>Madhumuni</u>. Makubaliano haya yanatawala uhusiano na ushirika wa kibiashara kati ya (a) Grubhub na (b) Mshirika wa Ufikishaji na waajiriwa, wanakandarasi, wanakandarasi wadogo, maajenti na wawakilishi wowote wa Mshirika wa Ufikishaji na watoa huduma ya ufikishaji wengine wanaohusishwa na Mshirika wa Ufikishaji ili kutekeleza Huduma za Ufikishaji kwa wateja (kwa pamoja, "Wanakandarasi Wadogo"). "Wanakandarasi Wadogo" pia inajumuisha waajiriwa, wanakandarasi, wanakandarasi wadogo, maajenti na wawakilishi wowote wa watoa huduma ya ufikishaji wengine wanaohusishwa na Mshirika wa Ufikishaji ili kutekeleza Huduma za Ufikishaji. Ili kufanikisha ahadi zilizo kwenye Makubaliano haya, Mshirika wa Ufikishaji atakuwa na haki ya kimkataba ya kutekeleza Huduma za Ufikishaji kulingana na Makubaliano haya, na kupokea Ada za Huduma zitakazokubalianwa na Wahusika.

2. <u>Uwakilisho na Uhakikisho wa Mshirika wa Ufikishaji</u>.

    a. Mshirika wa Ufikishaji anawakilisha na kutoa uhakikisho kwa yafuatayo:

        i. <u>Mahitaji ya Kisheria</u>. Mshirika wa Ufikishaji anahusika katika biashara au kazi huru ya kutoa Huduma za Ufikishaji zilizobainishwa na Makubaliano haya, na huduma hizo si biashara ya kawaida ya Grubhub na zinatekelezwa nje ya maeneo yote ya biashara ya Grubhub. Mshirika wa Ufikishaji ana leseni, vibali, na hati zote za usajili zinazohitajika ili kutekeleza Huduma za Ufikishaji katika eneo au maeneo ("Soko/Masoko") ambayo Mshirika wa Ufikishaji anachagua kutekeleza Huduma za Ufikishaji. Mshirika wa Ufikishaji anawajibika pekee katika kubainisha jinsi anavyoendesha biashara yake na kutekeleza Huduma za Ufikishaji.

        ii. <u>Umri na Leseni</u>. Mshirika wa Ufikishaji ana umri wa angalau miaka 18 na amekuwa na leseni halali ya dereva kwa angalau miaka 2, na ana kiwango mwafaka cha uhitimu unaohitajika au unaopendekezwa wa kuendesha gari linalotumika kutekeleza Huduma za Ufikishaji.

        iii. <u>Rekodi ya Kuendesha Gari</u>. Mshirika wa Ufikishaji ana rekodi ya kuendesha gari kwa usalama (ikiwa Mshirika wa Ufikishaji anatekeleza Huduma za Ufikishaji akitumia gari kama vile motokaa, pikipiki au skuta).

        iv. <u>Vifaa</u>. Mshirika wa Ufikishaji anadumisha kwa gharama zake mwenyewe vifaa vyote vinavyohitajika ili kutekeleza Huduma za Ufikishaji. Mshirika wa Ufikishaji hahitajiki kununua, kukodisha, au kupangisha vifaa vyovyote kutoka kwa Grubhub. Mshirika wa Ufikishaji anathiitisha kwamba vifaa vyako vinatimiza viwango vyote vya sekta na kiudhibiti, na vitakuwa katika hali nzuri ya kufanya kazi. Mshirika wa Ufikishaji anawajibikia pekee kuhakikisha kwamba gari lolote linalotumiwa linaambatana na sheria zote husika katika usajili, usalama, na ukaguzi.

v. Bima na Ushuru. Mshirika wa Ufikishaji anadumisha kwa gahrama zake mwenyewe bima za aina na viwango vilivyobainishwa hapa chini:

1. Ikiwa Mshirika wa Ufikishaji anatekeleza Huduma za Ufikishaji akitumia gari, basi Mshirika wa Ufikishaji atadumisha bima ya gari kwa kila gari linalotumiwa kutekeleza Huduma za Ufikishaji. Bima hiyo ya gari ni lazima iwe bima tosha kusimamia masuala yote yanayoibuka kuhusiana na Huduma za Ufikishaji, na ni lazima itimize vigezo vyote husika vya bima vya jimbo au ndani (ikijumuisha viwango vya chini zaidi vya bima). Grubhub inahifadhi haki ya kuagiza itajwe kama aliyesimamiwa na bima kwenye bima yoyote inayohitajika hapa. Mshirika wa Ufikishaji anaelewa kwamba unapotoa Huduma za Ufikishaji pamoja na Grubhub, bima yako binafsi ya gari huenda inakosa kugharimia dhima, kikamilifu, ajali, malipo ya matibabu, majeraha ya kibinafsi, mwendeshaji gari ambaye hana bima, mwendeshaji gari aliye na bima isiyotosha, au masuala mengine. Ikiwa Mshirika wa Ufikishaji ana maswali au wasiwasi zozote kuhusu wigo au utumikaji wa bima yako binafsi, ni wajibu wa Mshirika wa Ufikishaji kusuluhisha hayo na mtoa bima wako.

2. Mshirika wa Ufikishaji atadumisha bima ya fidia ya wafanyikazi inayosimamia watu wowote wanaotekeleza Huduma za Ufikishaji zilizobainishwa hapa, mradi iwe kwamba bima hiyo ya ajali kazini inaweza kudumishwa sambamba na bimaya fidia ya wafanyikazi kwa kiwango kinachoruhusiwa na sheria. Mshirika wa Ufikishaji anatambua kwamba Mshirika wa Ufikishaji hatastahiki kupokea mafao ya fidia ya wafanyikazi kupitia Grubhub na badala yake anawajibikia kudumisha bima ya Mshirika wa Ufikishaji binafsi ya fidia ya wafanyikazi. Mshirika wa Ufikishaji kudumisha bima ya Mshirika wa Ufikishaji binafsi ya fidia ya wafanyikazi haimzuia Mshirika wa Ufikishaji kushiriki katika bima fulani za makundi ambazo huenda zikawekwa na Grubhub na/au watoa bima wengine kwa ajili ya Mshirika wa Ufikishaji.

3. Kwa kiwango kinachohitajika na sheria husika, Mshirika wa Ufikishaji anawajibikia kuchukua na kulipia bima ya ulemavu, bima ya afya, na/au afya nyingine sawa; na bima zote hitajika za dhima. Mshirika wa Ufikishaji anawajibikia pekee kulipia bima ya afya, Mshirika wa Ufikishaji huenda akahitimu kupata punguzo kwenye huduma za afya kulingana na kanuni ya California Business and Professions Code § 7454.

4. Mshirika wa Ufikishaji anaelewa na kukubali kwamba Mshirika wa Ufikishaji hana haki ya kupata mafao ya bima ya kukosa ajira isipokuwa iwe bima ya fidia ya kukosa ajira inatolewa na Mshirika wa Ufikishaji au mhusika mwingine kando na Grubhub. Mshirika wa Ufikishaji pia anaelewa na kukubali kwamba Mshirika wa Ufikishaji ana jukumu la kulipa ushuru wa kitaifa na jimbo kwenye pesa zinazolipwa kulingana na Makubaliano haya.

5. Mshirika wa Ufikishaji anakubali kutoa ushahidi wa bima baada ya kuombwa. Mshirika wa Ufikishaji anakubali kutoa ushahidi ulisosasishwa wa bima kila wakati inapoweka upya au inapobadilisha bima hiyo baada ya kuombwa. Ni lazima Mshirika wa Ufikishaji apatie Grubhub ilani kwa maandishi angalau siku 30 kabla ya kughairi bima yoyote iliyobainishwa hapa.

b. Mshirika wa Ufikishaji ataarifu Grubhub maramoja endapo yoyote ya uwakilisho na uhakikisho uliotajwa si kweli tena.

c. Mshirika wa Ufikishaji anatambua kwamba wakati wa kutengeneza na kusajilisha akaunti, Grubhub itakusanya na inaweza kuthibitisha maelezo fulani kuhusu Mshirika wa Ufikishaji na, ikiwa inahusika, gari/magari ya Mshirika wa Ufikishaji yanayotumika kutoa Huduma za Ufikishaji. Mshirika wa Ufikishaji pia anatambua kwamba huenda akapitia kaguzi za mara kwa mara za historia na ripoti ya gari kulingana na sheria husika, na anaweza kuhitajika kutia ushahidi wa leseni, vifaa au bima baada ya kuombwa, ili Grubhub iweze kuthibitisha kwamba Mshirika wa Ufikishaji anaendelea kutimiza vigezo vya ustahiki vilivyobainishwa hapa.

d. Endapo yoyote ya uwakilisho na uhakikisho uliotajwa si kweli tena (“Kutostahiki”), Grubhub inaweza kusimamisha mara moja Huduma za Ufikishaji za Mshirika wa Ufikishaji na uwezo wa kufikia Programu ya Driver (kama ilivyobainishwa hapa chini) mpaka hali hiyo ya Kutostahiki kusuluhishwa. Grubhub inaweza kubatilisha Makubaliano haya ikiwa hali hiyo ya Kutostahiki haitasuluhishwa ndani ya siku 30 baada ya kupokea ilani kuhusu hali hiyo ya Kutostahiki au ikiwa hali hiyo ya Kutostahiki haiwezi kusuluhika.

3. Matumizi ya Programu ya Driver. Mshirika wa Ufikishaji anatambua kwamba utekelezaji wa Huduma za Ufikishaji chini ya Makubaliano haya unahitaji matumizi ya programu ya simu ya Grubhub (“Programu ya Driver”), na kwamba ikiwa Mshirika wa Ufikishaji hawezi kufikia au kutumia Programu ya Driver, Mshirika wa Ufikishaji hataweza kutekeleza Huduma za Ufikishaji chini ya Makubaliano haya. Matumizi ya Programu ya Driver si sharti kwa Mshirika wa Ufikishaji baada ya kukubali Shughuli yoyote maalum (kama ilivyobainishwa hapa chini).

   a. Unaweza tu kutumia Programu ya Driver ikiwa wewe ni Mshirika wa Ufikishaji aliyeidhinishwa na Grubhub (“Mshirika wa Ufikishaji”) kwa Makubaliano ya Mshirika wa Ufikishaji ya sasa na yaliyotiwa sahihi kwa njia halali, na kwa malengo tu ya kutekeleza Huduma za Ufikishaji. Haki na uwezo wako wa kuendelea kutumia Programu ya Driver kwa malengo ya kutekeleza Huduma za Ufikishaji itabatilishwa mara moja Makubaliano yako ya Mshirika wa Ufikishaji yakibatilishwa.

   b. Matumizi ya Programu ya Driver yanakuhitaji usajilishe na/au utengeneze akaunti (“Akaunti”) kwa kupatiana maelezo fulani ya kibinafsi. Katika uzingatiaji wa matumizi ya Programu ya Driver, Wewe unakubali: (a) kupatiana maelezo ya kweli, sahihi, ya sasa, na kamilifu kukuhusu wewe mwenyewe kama inavyoagizwa na fomu ya usajili; na (b) kudumisha na kusasisha bila kuchelewa maelezo ya kibinafsi unayopatiana ili kuhakikisha kwamba yanasalia kuwa ya kweli, sahihi, ya sasa, na kamilifu. Hauwezi kutengeneza Akaunti zaidi ya moja.

   c. Una wajibu wa kudumisha faragha na usalama wa Akaunti yako na nenosiri lako, na shughuli zote na matendo mengine yoyote yanayofanyika kwenye au kufanywa kuhusiana na nenosiri lako au Akaunti yako. Unakubali kulinda na kuweka faraghani njia zozote za kuingia kwenye Akaunti yako kupitia Programu ya Driver kwa kutekeleza hatua mwafaka za kiufundi na kimpangilio. Unatambua kwamba matumizi bila idhini ya Akaunti yako kunaweza kupelekea hasara za kifedha na ufikiaji wa maelezo nyeti ya kibinafsi yako na ya Akaunti yako. Ukifichua maelezi ya Akaunti yako au njia za kuingia kwenye Akaunti yako kwa mtu au mhusika yeyote, Wewe utawajibikia hatari na hasara zote zinazohusiana na ufichuaji huo. Unakubali (a) kuarifu Grubhub mara moja kuhusu matumizi yoyote yanayojulikana au kudhaniwa kuwa bila idhini ya nenosiri lako au Akaunti yako, au ukiukaji wowote unaojulikana au unaodhaniwa wa usalama, pamoja na hasara, wizi, au ufichuaji bila idhini wa nenosiri lako au Akaunti yako kupitia Programu ya Driver; na (b) kuhakikisha kwamba unatoka kwenye Akaunti yako kila baada ya kipindi cha kutumia. Grubhub haitawajibikia jeraha lolote, hasara yoyote au uharibifu wowote wa aina yoyote unaotokana au kuhusiana na wewe kukosa kuambatana na (a) au (b) hapa juu, au kwa ajili ya matendo yoyote yako au ya mtu mwingine anayetumia Akaunti yako na/au nenosiri lako.

   d. Eneo. Mshirika wa Ufikishaji anatambua na kukubali kwamba maelezo ya eneo la kijiografia ya kifaa chako yanayotumiwa ili kufikia Programu ya Driver ni lazima yapatianwe kwa Grubhub kupitia Programu ya Driver ili kutoa Huduma za Ufikishaji, na kwamba maelezo hayo ya eneo la kijiografia huenda yakafuatiliwa na Grubhub na kusambazwa kwa wahusika wengine wakati Mshirika wa Ufikishaji amaeinhia ndani na yuko tayari kupata ofa za Huduma za Ufikishaji kupitia Programu ya Driver. Mshirika wa Ufikishaji hataripoti eneo lake la kijiografia kwa udanganyifu, hatazui wala kujaribu kuzuia Programu ya Driver kuripoti eneo lake la kijiografia au vinginevyo kujaribu kuepuka kigezo hiki.

   e. Usalama. Mshirika wa Ufikishaji anakubali kwamba, ili kuambatana na sheria, masharti, na kanuni zote husika za kitaifa, jimbo, na ndani, Grubhub inaweza ikahitaji kwamba Mshirika wa Ufikishaji akamilishe mafuno ya lazima ya kiusalama yanayotolewa na Grubhub au mchuuzi mwingine kabla ya Mshirika wa Ufikishaji awezeshwe kutumia Mfumo (ikijumuisha Programu ya Driver) au Mshirika wa Ufikishaji aweze kuendelea kuutumia. Aidha, Mshirika wa Ufikishaji anakubali kwamba, kulingana na sheria husika, mara kwa mara katika kipindi cha Makubaliano haya, Grubhub inaweza kuhitaji kwamba Mshirika wa Ufikishaji akubali mafunzo ya usalama ya ziada. Mshirika wa Ufikishaji vinginevyo hatahitajika kufanya mafunzo yoyote.

4. Huduma za Ufikishaji. Grubhub italipa Mshirika wa Ufikishaji Ada ya Huduma kwa ajili ya ufikishaji uliokamilishwa. Mbinu ya kufanya na/au kukubali ofa ya Ada ya Huduma ili kukamilisha ufikishaji (“Ofa ya Ada”) (k.m. kwa barua pepe au kupitia Programu ya Driver) inaweza kubadilika mara kwa mara kwa hiari ya Grubhub, mradi iwe Grubhub inakubali kuwasilisha mbinu hiyo kwa Mshirika wa Ufikishaji. Mshirika wa Ufikishaji anakubali kuipatia Grubhub anwani yako ya barua pepe, na anakubali kuarifu Grubhub wakati wowote anwani hiyo inabadilika. Mshirika wa Ufikishaji ana hiari ya kuchagua ni Ofa zipi za Ada anaweza kukubali na ni zipi hawezi kukubali.

Mshirika wa Ufikishaji akiamua kukubali Ofa fulani ya Ada, Mshirika wa Ufikishaji anakubali kutekeleza Huduma za Ufikishaji za Ofa hiyo ya Ada ("Shughuli") kulingana na sehemu ndogo ya (a) hapa chini. Mshirika wa Ufikishaji ana hiari ya kama atatekeleza, wakati gani atatekeleza, na mara ngapi atatekeleza Shughuli hizo. Mshirika wa Ufikishaji akiamua kutokubali Ofa ya Ada, Mshirika wa Ufikishaji hana jukumu la kutekeleza Huduma za Ufikishaji zinazoagizwa na Shughuli inayopendekezwa. Hajuna chochote ndani ya Makubaliano haya kinamlazimu Mshirika wa Ufikishaji kutekeleza Shughuli yoyote fulani au idadi yoyote maalum ya Shughuli.

a. Katika kipindi cha Shughuli yoyote, Mshirika wa Ufikishaji anakubali kutekeleza Huduma za Ufikishaji kwa namna ya kitaalamu ambayo angalau inalingana na viwango vya sekta, ikijumuisha lakini si tu yafuatayo:

    i. Mshirika wa Ufikishaji anakubali kuchukua kila oda kutoka kwa Muuzaji bila kuchelewa na kwa namna ya kitaalamu. Mshirika wa Ufikishaji anakubali kuambatana na utambulisho wote unaoeleweka na vigezo vingine vinavyowekwa na Wauzaji.

    ii. Mshirika wa Ufikishaji anakubali kufikisha oda kwa wateja bila kuchelewa na kwa namna ya kitaalamu. Mshirika wa Ufikishaji anakubali kufuata maagizo yanayoeleweka yanayotolewa na mteja.

    iii. Mshirika wa Ufikishaji anakubali kuarifu Grubhub kuhusu masuala yoyote ya Muuzaji au mteja, ikijumuisha lakini si tu makosa kwenye oda yoyote ya chakula au kwenye anwani yoyote ya ufikishaji iliyowekwa.

    iv. Mshirika wa Ufikishaji anakubali kutumia Programu ya Driver ili kuwasilisha hali ya oda kwa Wauzaji na/au wateja, ikijumuisha kukubali oda au ofa za safari, kufika kwa Muuzaji, kupokea chakula na kukamilisha ufikishaji. Mshirika wa Ufikishaji anatambua kwamba Programu ya Driver inaweza kusasishwa mara kwa mara, na aina na wakati wa mawasiliano unaweza kubadilika. Ikiwa kuna masuala kwenye Programu ya Driver, Mshirika wa Ufikishaji ana wajibu wa kuarifu Grubhub bila kuchelewa, na Grubhub inaweza kumkataza Mshirika wa Ufikishaji kutekeleza Huduma za Ufikishaji mpaka wakati Programu inafanya kazi vizuri.

    v. Mshirika wa Ufikishaji anakubali kwamba Huduma za Ufikishaji zitafanywa kwa namna salama na kulingana na sheria, kanuni, na miongozo zote husika za trafiki. Mshirika wa Ufikishaji anakubali kutotekeleza Huduma za Ufikishaji akiwa mlevi, na kutokunywa vinjwaji vya pombe ndani ya muda unaoeleweka kabla ya kuhusika katika, au wakati wowote anapotoa, Huduma za Ufikishaji chini ya makubaliano haya. Mshirika wa Ufikishaji anatambua kwamba uwezo wake wa kufikia Programu ya Driver utasimamishwa na kusubiri uchunguzi ikiwa Grubhub itapokea ripoti kwamba Mshirika wa Ufikishaji anadhaniwa kwa sababu tosha kuwa ni mlevi wa dawa za kulevya au pombe akiwa angali anatoa Huduma za Ufikishaji chini ya Makubaliano haya.

    vi. Mshirika wa Ufikishaji anakubali kudumisha na kutumia vifaa vyote vinavyohitajika ili kutekeleza Huduma za Ufikishaji. Mshirika wa Ufikishaji anatambua kwamba bili kipimo kwa yaliyotajwa hapa juu, vifaa vifuatavyo vinahitajika ili kutekeleza Huduma za Ufikishaji:

        1. Gari au baiskeli, kama inavyokubalianwa kati ya Gribhub na Mshirika wa Ufikishaji. Gari au baiskeli hiyo ni lazima isajiliwe ifaavyo ili kutekeleza Huduma a Ufikishaji katika Soko/Masoko kwa njia ya kisheria.

        2. Simu maizi iliyounganishwa na wavuti yenye mpango wa data na kamera inayofanya kazi kwa ajili ya ufikishaji bila kugusana na kuskani vitambulisho kwa Washirika wa Ufikishaji ambao wanafanya ufikishaji unaohusisha pombe. Ufikikiaji wa mtandao ni lazima kwa ujumla upatikane nyakati zote huku Mshirika wa Ufikishaji anapotekeleza Huduma za Ufikishaji. Ufikiaji wa data wa WIFI pekee hautoshi. Simu hiyo maizi haiwezi kufanyiwa mchakato wa "jailbreak" (ikiwa ni iPhone au ) au "root" (ikiwa ni Android), au vinginevyo kubadilishwa ili kuhepa vigezo au michakato ya Programu ya Driver. Mshirika wa Ufikishaji anakubali kuwasiliana na Wauzaji na/au wateja kwa namna ya kiutaalamu na hatawasiliana na wateja au Wauzaji zaidi ya inavyohitajika ili kutimiza Huduma ya Ufikishaji.

        3. Mifuko maalum ya ufikishaji. Mshirika wa Ufikishaji anaweza, lakini si lazima akubali, kukodisha au kununua mifuko maalum ya ufikishaji kutoka kwa Grubhub kwa mpango tofauti na Grubhub.

    vii. Mshirika wa Ufikishaji hahitajiki kuvaa sare yoyote, au kutumia, kuvaa, au kuonyesha vitu ana alama zenye nembo ya Grubhub mwilini mwake au kwenye gari lake wakati wowote. Hata hivyo,

Mshirika wa Ufikishaji anakubali kudumisha mwonekano wa kitaalamu sambamba na viwango vya sekta.

viii. Grubhub inaweza kumpa Mshirika wa Ufikishaji kadi moja au zaidi ya kulipiwa kwanza kwa malengo ya kulipia oda kutoka kwa Muuzaji ("Kadi ya Malipo"). Mshirika wa Ufikishaji anatambua kwamba Kadi hizo za Malipo zinatolewa tu ili kuwezesha oda zilizowekwa na mteja kwa biashara fulani zinazohitaji Mshirika wa Ufikishaji kuweka oda hiyo mwenyewe, kulingana na makubaliano kwa maandishi au inaporuhuiwa na sheria. Mshirika wa Ufikishaji anakubali kuamilisha bila kuchelewa Kadi hiyo ya Malipo inayopanwa na Grubhub. Mshirika wa Ufikishaji anakubali kwamba Kadi hiyo ya Malipo si ya matumizi au gharama za kibinafsi za Mshirika wa Ufikishaji. Mshirika wa Ufikishaji anakubali kutumia tu Kadi hiyo ya Malipo kulipia oda zilizowekwa na mteja kwenye Mfumo na kuchaguliwa na Mshirika wa Ufikishaji ili kumpa mteja huyo Huduma ya Ufikishaji na kwa kiwango tu cha oda hiyo. Mshirika wa Ufikishaji anatambua na kuelewa kwamba Grubhub inaweza, kwa hiari yake, kusimamisha leseni ya Mshirika wa Ufikishaji ya kutuma Programu ya Driver mpaka wakati Kadi ya Malipo inapoamilishwa. Ikiwa Mshirika wa Ufikishaji hajaamilisha Kadi ya Malipo ndani ya siku 14 baada ya kuipokea, Grubhub inaweza kubatilisha Makubaliano haya baada ya ilani ya maandishi kwa Mshirika wa Ufikishaji.

b. Isipokuwa ikubalianwe vinginevyo kati ya Grubhub na Mshirika wa Ufikishaji au vinginevyo inavyohitajika na sheria, Grubhub haina jukumu la kulipa Mshirika wa Ufikishaji Ada zozote za Huduma au malipo mengine ambayo Mshirika wa Ufikishaji anaweza kuwa na haki ya kupokea kutoka kwa Grubhub ambayo yanahusishwa na oda ambazo hazijakamilishwa katika uambatanaji mkubwa na sehemu ndogo ya (a) hapa juu. Mshirika wa Ufikishaji hatahepa au kujaribu kuhepa masharti au vigezo vya Sehemu hii ya 4.

c. Ili kuambatana na Makubaliano haya (pamoja na ahadi za kiwango cha huduma zilizobainishwa katika Sehemu hii ya 4), Mshirika wa Ufikishaji atawajibika pekee katika kubaini jinsi ya kutekeleza Hudumza za Ufikishaji, ikijumuisha lakini si tu kama atatumia Wanakandarasi Wadogo ili kutekeleza sehemu ya Huduma za Ufikishaji au zote, na Grubhub haitakuwa na haki yoyote, na haitadhibiti au kuagiza namna, mbinu, au njia ambazo Mshirika wa Ufikishaji anatumia ili kukamilisha Huduma za Ufikishaji, pamoja na kutathmini ubora wa Huduma za Ufikishaji za Mshirika wa Ufikishaji au kumwagiza Mshirika wa Ufikishaji jinsi ya kutekeleza Huduma za Ufikishaji, au kubaini namna ya kuchukua, kufikisha, na kuchagua njia ya kupitia (mradi iwe njia iliyochaguliwa haihitilafiani na ukamilishaji wa Shughuli bila kuchelewa na kwa njia ya kiutalaamu). Aidha, Mshirika wa Ufikishaji hatakuwa na msimamizi au meneja yeyote, au mtu mwingine yeyote wa Grubhub ambaye Mshirika wa Ufikishaji anahitajika kuripoti kwake. Kauli za Makubaliano haya zinazohifadhi mamlaka thabiti ya Grubhub zimewekwa tu kwa ajili ya kufanikisha uambatanaji na sheria, kanuni na tafsiri za kitaifa, jimbo, au za ndani.

d. Hakuna kitu chochote hapa kitamzuia Mshirika wa Ufikishaji kutoa huduma kwa biashara nyingine yoyote, pamoja na biashara zinazoshindana moja kwa moja na Grubhub. Huduma hizo zinaweza kutekelezwa sambamba na Huduma za Ufikishaji wakati wa Shughuli, mradi iwe kwamba huduma hizo sambamba hazizuii Mshirika wa Ufikishaji kutekeleza Huduma za Ufikishaji wakati wa Shughuli kama hiyo. Hakuna kitu chochote hapa kitamzuia Mshirika wa Ufikishaji kufanya uhusiano wa kibiashara wa moja kwa moja na Wauzaji au wateja.

e. Mshirika wa Ufikishaji anaelewa na kukubali kwamba vigezo vya kila Huduma ya Ufikishaji vinawekwa na mteja na/au Muuzaji, si Grubhub, na vinawakilisha tokeo linalotakikana, si kwa mbinu ambazo Mshirika wa Ufikishaji atafanikisha tokeo. Mshirika wa Ufikishaji ana haki ya kughairi Huduma ya Ufikishaji wakati, katika kutekeleza faragha na maamuzi ya kibiashara ya Mshirika wa Ufikishaji, ni mwafaka kufanya hivyo. Bila kujali yaliyotajwa hapa juu, Mshirika wa Ufikishaji anakubali kudumisha kadirio la mteja na kiwango cha ukamilishaji kama inavyobainishwa na Grubhub. Kukosa kutimiza jukumu hili ni ukiukaji mkubwa wa Makubaliano haya, na katika hapo Grubuhub itakuwa na haki ya kubatilisha Makubaliano haya na/au kufunga akaunti ya Mshirika wa Ufikishaji. Mshirika wa Ufikishaji hatajaribu kumpendekezea wala kumshawishi mteja au Muuzaji kughairi Huduma zozote za Ufikishaji.

f. Mshirika wa Ufikishaji anatambua na kukubali kwamba ana jukumu la kuambatana na sheria na kanuni husika zinazotumika kwenye utekelezaji wa Huduma za Ufikishaji kwa wateja (ikijumuisha kupitia matumizi ya Wanakandarasi Wadogo). Mshirika wa Ufikishaji ataambatana na sera na miongozo yote ya Grubhub kama inavyochapishwa au kuwasilishwa kwa Mshirika wa Ufikishaji mara kwa mara, pamoja na Kufikisha Pombe.

g. Kukosa kuambatana na sehemu yoyote ya Sehemu ya 4 ni ukiukaji mkubwa wa Makubaliano haya.

5. Ada za Huduma na Ankara.

a. Ada za Huduma. Grubhub italipa Mshirika wa Ufikishaji Ada za Huduma kwa ajiili ya Huduma za Ufikishaji kwa viwango na kulingana na makubaliano kati ya Wahusika kwa kila Shughuli.

b. Malipo ya Shukrani. Mshirika wa Ufikishaji atasalia 100% na malipo yoyote na yote ya shukrani anayopokea kutoka kwa wateja, iwe imepatianwa kama pesa taslimu au kulipwa kupitia Mfumo, na atapatiana malipo hayo ya shukrani kwa Wanakandarasi Wadogo wowote kulingana na sheria husika. Grubhub haihitajiki kukusanya kiwango cha chini zaidi cha malipo ya shukrani kutoka kwa wateja kwa kutumia Mfumo, au kupatiana malipo yoyote ya shukrani ambayo hayajapokewa au kuhifadhiwa kutoka kwa wateja.

c. Kiwango Kizima; Gharama. Ada za Huduma na malipo yoyote ya shukrani yanayolipwa na wateja kwa Mshirika wa Ufikishaji kulingana na Makubaliano haya yanajumuisha kiwango kizima cha kulipwa na Grubhub kwa ajili ya Mshirika wa Ufikishaji au Wanakandarasi Wadogo wowote kutekeleza Huduma za Ufikishaji. Mshirika wa Ufikishaji anatambua na kukubali kwamba anawajibikia pekee gharama zote zinazoibuka kutokana ana kutekeleza Huduma za Ufikishaji, ikijumuisha lakini si tu gharama zinazohusiana na Wanakandarasi Wadogo, vifaa, ukiukaji wa magari au ukiukaji kwenye matumizi ya mifumo mingine ya usafiri, na uharibifu au upotezaji mali. Isipokuwa ibainishwe vinginevyo na sheria husika, Mshirika wa Ufikishaji atakubali hatari zote za uharibikaji au upotezaji wa vifaa vyovyote vinavyotumiwa ili kutekeleza Huduma za Ufikishaji. Aidha, Mshirika wa Ufikishaji ana wajibu wa kuthibitisha usahihi wa akaunti yake ya benki na/au maelezo ya kadi yake ya salio ili kupokea malipo. Grubhub haiwajibikii malipo yaliyopotea au ylaiyochelewa kwa ajili ya maelezo ya malipo ambayo si sahihi.

d. Kuripoti. Grubhub itaripoti Ada zote za Huduma zinazolipwa kwa Mshirika wa Ufikishaji katika kalenda ya mwaka kwa kutumia Fomu ya IRS ya 1099 ikiwa kiwango cha malipo kwa Mshirika wa Ufikishaji kinahitimu. Mshirika wa Ufikishaji anakubali kuripoti malipo hayo yote kwa mamlaka mwafaka ya ushuru ya kitaifa, jimbo na ndani. Baada ya Makubaliano haya kutiwa sahihi, Mshirika wa Ufikishaji atapatia Grubhub nambari ya leseni yake ya biashara na nambari ya utabulisho wa mwajiriwa ya kitaifa (ikiwa ipo).

e. Migogoro. Malipo ya Grubhub kwa Mshirika wa Ufikishaji chini ya masharti ya Makubaliano haya yatachukuliwa kuwa kamilifu na sahihi isipokuwa mgogoro uibuke kulingana na vigezo vifuatavyo. Ili kuibua mgogoro kuhusu malipo, Mshirika wa Ufikishaji ni lazima awasilishe ilani ya mgogoro huo kwa Grubhub ndani ya siku 30 baada ya kupokea malipo. Ikiwa Wahusika hawawezi kusuluhisha mgogoro huo, mgogoro huo utawasilishwa kwa mchakato wa usuluhishaji kulingana na Sehemu ya 13 hapa chini.

6. Uhusiano wa Wahusika.

a. Makubaliano haya yanafanywa kati ya biashara mbili sawa na huru ambazo zinamilikiwa na kuendeshwa vitofauti. Wahusika wanakusudia Makubaliano haya kutengeneza uhusiano wa mwanakandarasi mkuu na huru kati ya Grubhub na Mshirika wa Ufikishaji, na si uhusiano wa mwajiri na mwajiriwa kwa malengo yoyote. Mshirika wa Ufikishaji na Grubhub si maajenti, wafanyibiashara wa pamoja, au washirika kati yao kwa malengo yoyote. Hakuna Mhusika atakuwa na haki ya kumfunga yule mwingine kwa mkataba au vinginevyo isipokuwa kama ilivyobainishwa hapa. Mshirika wa Ufikishaji anatambua kwamba Mshirika wa Ufikishaji anahusika katika biashara ya kibinafsi ya Mshirika wa Ufikishaji, kando na tofauti na biashara ya Grubhub, na anawakilisha na kutoa hakikisho kwamba inajionyeshana hadharani kama biashara iliyowekwa kitofauti.

b. Mshirika wa Ufikishaji anawakilisha na kutambua yafuatayo:

i. Mshirika wa Ufikishaji anaelewa kwamba Makubaliano haya ni msingi wa uhusiano wa mwanakandarasi mkuu na huru, si mwajiri na mwajiriwa.

ii. Mshirika wa Ufikishaji haswa anataka na anakusudia kujiendesha kama biashara huru inayotoa huduma za ufikishaji.

iii. Wakati wowote Mshirika wa Ufikishaji akiamini kwamba uhusiano wake na Grubhub ni wa aina

nyingine kando na uhusiano wa mwanakandarasi huru, Mshirika wa Ufikishaji anakubali kuarifu Grubhub mara moja kuhusu mtazamo huu.

c. Kwa kiwango ambacho Mshirika wa Ufikishaji anahusisha Mwanakandarasi yeyote Mdogo kutekeleza Huduma za Ufikishaji, Mshirika wa Ufikishaji na Grubhub wanatambua na kukubali kwamba Mwanakandarasi huyo Mdogo si mwajiriwa wa Grubhub na hakuna uhusiano wa ajira kati ya Mwanakandarasi Mdogo na Grubhub. Grubhub wala Mwanakandarasi Mdogo hatakuwa na haki ya kumfunga yule mwingine kwa mkataba au vinginevyo, isipokuwa kama ilivyobainishwa hapa.

7. Wanakandarasi Wadogo. Kwa kuambatana na Makubaliano haya (ikijumuisha vigezo vilivyobainishwa katika Sehemu hii ya 7 na ahadi za kiwango cha huduma zilizobainishwa katika Sehemu ya 4) na kwa kiwango kinachoruhusiwa na sheria, Mshirika wa Ufikishaji atakuwa na hiari ya kuchagua kutumia Wanakandarasi Wadogo, na anawajibikia uelekezaji na udhibiti wa Wanakandarasi wake Wadogo. Mshirika wa Ufikishaji (au mmiliki au mkuu wake) hana jukumu chini ya Makubaliano haya la kutekeleza Huduma zozote za Ufikishaji. Bila kujali yaliyotajwa, Mshirika wa Ufikishaji anasalia kuwa na dhima katika utekelezaji Huduma za Ufikishaji wa Wanakandarasi wake Wadogo, na kuhusishwa kwa Wanakandarasi Wadogo hakutamwondolea Mshirika wa Ufikishaji yoyote ya majukumu haya yaliyo hapa.

a. Ada za Huduma zinazofaa kulipwa kwa ajili ya Huduma za Ufikishaji zilizotekelezwa na Wanakandarasi Wadogo zitalipwa kwa Mshirika wa Ufikishaji. Mshirika wa Ufikishaji anachukua wajibu kamili, na Grubhub hautakuwa na wajibu, wa malipo ya fidia, mafao, na gharama zozote kwa Wanakandarasi Wadogo (ambayo yataamuliwa kwa hiari ya Mshirika wa Ufikishaji), na kwa ushikiliaji ushuru wowote, bima yoyote ya kukosa ajira, na ushuru wowote wa malipo ya uzeeni unaohitajika wa jimbo au kitaifa unaohusiana na Wanakandarasi Wadogo. Isipokuwa iwe inahitajika na sheria, Grubhub haitakuwa na majukumu yoyote ya kushikilia ushuru unaohusiana na fidia kwa Wanakandarasi Wadogo.

b. Mshirika wa Ufikishaji akitumia huduma za Mwanakandarasi yeyote Mdogo ili kutekeleza Huduma za Ufikishaji, Mwanakandarasi Mdogo wa Mshirika wa Ufikishaji ni lazima atimize na kuambatana na masharti ya Makubaliano haya, jambo ambalo Mshirika wa Ufikishaji ni lazima awezeshe kutekelezeka kwa kutumia makubaliano kwa maandishi kati ya Mshirika wa Ufikishaji na Mwanakandarasi huyo Mdogo. Nakala ya makubaliano hayo kwa maandishi ni lazima ipatianwe kwa Grubhub angalau siku 7 mbele kabla ya Mwanakandarasi huyo Mdogo kutekeleza Huduma za Ufikishaji, na Mshirika wa Ufikishaji ni lazima aarifu Grubhub wakati ambao Mwanakandarasi wake Mdogo atatekeleza Huduma za Ufikishaji. Wahusika wanatambua kwamba lengo pekee la kigezo hiki ni kuhakikisha Mshirika wa Ufikishaji anaambatana na masharti ya Makubaliano haya.

8. Uondoaji Lawama.

a. Mshirika wa Ufikishaji anakubali kuiondolea lawama, kuilinda, na kuichukulia Grubhub isiyodhuru pamoja na washirika wake, na waajiriwa, maafisa, wakurugenzi, na maajenti wake (kwa pamoja, “Wanaoondolewa Lawana na Grubhub”) dhidi ya madai, kesi, hasara, kesi, dhima, uharibifu, na gharama (ikijumuisha ada za wakili zinazoeleweka) zinazoibuka moja kwa moja au vinginevyo, kutokana au kuhusiana na (i) matendo ya Mshirika wa Ufikishaji, Mwanakandarasi yeyote Mdogo ai mtu mwingine aliyeajiriwa au kuhusishwa na Mshirika wa Ufikishaji, ikijumuisha lakini si tu uharibifu wa mali au jeraha la kibinafsi la, au kifo cha, mtu yeyote, au (ii) Mshirika wa Ufikishaji au Wanakandarasi wake Wadogo au mtu mwingine aliyeajiriwa au kuhusishwa na Mshirika wa Ufikishaji kukukosa kuambatana na masharti ya Makubaliano haya. Grubhub itakuwa na haki ya kuchagua mshauri wake na kuelekeza utetezi wake endapo kuna dai linalofanywa linaloamilisha haki yake ya kuondolewa lawama. Majukumu ya Mshirika wa Ufikishaji hapa yatajumuisha gharama za utetezi, ikijumuisha ada za wakili. na pia malipo ya uamuzi wowote wa mwisho unaotolewa dhidi ya au fidia iliyokubalianwa na Wanaoondolewa Lawama na Grubhub.

b. Mshirika wa Ufikishaji anakubali kuondolea lawama, kulinda na kuchukulia Wanaoondolewa Lawama na Grubhub kuwa wasiodhuru dhidi ya dhima zote za ushuru na majukumu yote ya kulipa ushuru wa kitaifa, jimbo na ndani, ikijumuisha lakini si tu ushuru wote wa mishahara, ushuru wa ajira ya kibinafsi, malipo ya fidia ya wafanyikazi, na michango mingine yoyote iliyowekwa au inayohitajika chini ya sheria za kitaifa, jimbo, mkoa, na ndani kuhusiana na Mshirika wa Ufikishaji na Wanakandarasi wowote Wadogo.

c. Mshirika wa Ufikishaji anakubali kuondolea lawama, kulinda na kuchukulia Wanaoondolewa Lawama na Grubhub kuwa wasiodhuru dhidi ya gharama na majukumu yote ya biashara ya Mshirika wa Ufikishaji ambayo yanapaswa kulipwa na Grubhub, ikijumuisha lakini si tu gharama za mishahara (au mishahara ya myuma), mafao ya waajiriwa, bima, au leseni za kiudhibiti, vibali, faini, na tathmini za mashirika, bodi, na manispaa yoyote na zote ya kiudhibiti.

d. Isipokuwa isuluhishwe kwa njia isiyo rasmi au katika mahakama ndogo za madai, au isipokuwa Mshirika wa Ufikishaji awe amejiondoa kwenye Kauli ya Usuluhishaji wa Pamoja, madai yote ya hasara au jeraha kati ya Grubhub na Mshirika wa Ufikishaji yatasuluhishwa kulingana na Kauli ya Usuluhishaji wa Pamoja (kama ilivyobainishwa katika Sehemu ya 13).

9. <u>KIPIMO CHA DHIMA</u>. KWA KIWANGO KINACHORUHISIWA NA SHERIA HUSIKA, GRUBHUB HAINA DHIMA AU WAJIBU KWA: (A) JERAHA LA KIBINAFSI (IKIJUMUISHA KIFO) AU UHARIBIFU WA MALI, WA AINA YOYOTE ILE, KUHUSIANA NA UTEKELEZAJI WA HUDUMA ZA UFIKISHAJI AU UFIKIAJI AU MATUMIZI YA PROGRAMU YA DRIVER; (B) HITILAFU, MAKOSA AU KASORO KWENYE PROGRAMU YA DRIVER; (C) KUDAKIZWA AU KUSITISHWA KWA UWASILISHAJI KWA AU KUTOKA KWA PROGRAMU YA DRIVER; (D) HITILAFU KATIKA MAUDHUI YOYOTE; (E) VIRUSI AU VITU VINGINE KAMA HIVYO AMBAVYO VINAWEZA KUTUMWA KWA AU KUPITIA PROGRAMU YA DRIVER; AU (F) UFIKIAJI AU MATUMIZI BILA IDHINI YA SEVA ZA GRUBHUB NA/AU MAELEZO YOYOTE NA YOTE YA KIBINAFSI YALIYOHITAFDHIWA PALE NA MHUSIKA MWINGINE YEYOTE..

10. <u>Mchakato wa Kisheria Unaoathiri Akaunti ya Mshirika wa Ufikishaji.</u>

a. Ikiwa hatua ya kisheria, kama vile kupokonywa mali ili kulipa deni, ada, adhabu, faini au mchakato mwingine wa kisheria wa jimbo, ndani au kitaifa ("Mchakato wa Kisheria") unaletwa dhidi ya akaunti ya Mshirika wa Ufikishaji, Grubhub haitapinga Mchakato wowote kama huo wa Kisheria kwa niaba ya Mshirika wa Ufikishaji. Grubhub inaweza kuchukua hatua dhidi ili kuambatana na Mchakato kama huo wa Kisheria ambao Grubhub inabaini kuwa mwafaka katika hali husika bila dhima yoyote kwa Mshirika wa Ufikishaji, ikijumuisha kushikilia viwango kutoka kwa Huduma za Ufikishaji ambazo vinginevyo vingewasilishwa kwa Mshirika wa Ufikishaji ili kusimamia Mchakato kama huo wa Kisheria. Mshirika wa Ufikishaji anakubali kwamba Grubhub inaweza kuheshimu Mchakato wa Kisheria ambao inakabidhiwa, kwa barua pepe au faksi katika kituo chochote cha Grubhub au baada ya ajenti yeyote aliyeidhinishwa kwa uteuzi au na sheria kupokea kwa niaba ya Grubhub, hata kama upokeaji huo hautoshi kisheria. Mchakato wa Kisheria ukiletwa dhidi ya akaunti ya Mshirika wa Ufikishaji, Grubhub inaweza kumzuia Mshirika wa Ufikishaji kutumia mbinu za malipo kando na uwekaji fedha wa moja kwa moja wa kila siku (yaani, kupinga matumizi ya Instant Cash Out au mbinu zingine mbadala za malipo ambazo Grubhub inaweza kumpa Mshirika wa Ufikishaji). Mshirika wa Ufikishaji atakuwa na dhima kwa Grubhub kwa ajili ya viwango vyovyote vinavyopokewa na Mshirika wa Ufikishaji kupitia mbinu za malipo kando na uwekaji fedha wa moja kwa moja wa kila wiki ambao vinginevyo ungesimamishwa kulingana na Mchakato huo wa Kisheria, na Grubhub inaweza kurejesha au kuondoa viwango hivyo kutoka kwa majukumu ya Grubhub kwa Mshirika wa Ufikishaji. Mshirika wa Ufikishaji anatambua kwamba Mchakato huo wa Kisheria dhidi ya akaunti ya Mshirika wa Ufikishaji ya Grubhub unaweza kupelekea kuchelewa kwa malipo kwa Mshirika wa Ufikishaji. Grubhub haitakuwa na dhima kwa Mshirika wa Ufikishaji kuhusiana na hasara zozote zinazotokana na kuchelewa huko. Aidha, kwa kiwango ambacho Grubhub inalipa kiwango cha fedha kwa wahusika wengine kutokana na tabia ya Mshirika wa Ufikishaji, Grubhub imeidhinishwa kushikilia viwango hivyo kutoka kwenye malipo ya Mshirika wa Ufikishaji ambayo anatarajia kutokana na kutekeleza Huduma za Ufikishaji.

11. <u>Faragha na Vikwazo vya Kutumia Maelezo ya Kibinafsi</u>.

a. <u>Maelezo ya Faraghani</u>. Wahusika wanaelewa kwamba uhusiano wa mwanakandarasi huru unaotengenezwa na Makubaliano haya unahitaji Wahusika kufichua na kubadilishana maelezo ya faraghani, yenye hakimiliki, na mengine nyeti au ambayo hayapatikani hadharani kuhusiana na operesheni au wateja wao (kwa pamoja, "Maelezo ya Faraghani"). Maelezo ya Faraghani ya Grubhub yanajumuisha lakini si tu: (i) maelezo ya mawasiliano ya washirika Wauzaji wa Grubhub; (ii) maelezo ya

kibinafsi ya wateja kama vile barua pepe, nambari ya simu, na anwani); (iii) taratibu za ada na bili; (iv) mipango ya kimkakati; (v) nyenzo za uuzaji na utangazaji; (vi) data kuhusiana na mbinu, fomula, mifumo, michakato ya data na teknolojia; na (vii) makubaliano, ilani, na mawasiliano mengine kati ya Grubhub na Mshirika wa Ufikishaji. Maelezo ya Faraghani ya Mshirika wa Ufikishaji yanajumuisha lakini si tu: (i) vifaa; (ii) leseni na idhini nyingine za kisheria; (iii) operesheni za kibiashara; (iv) orodha ya wateja wa Mshirika wa Ufikishaji; na (v) nyenzo za uuzaji na utangazaji.

b. Matumizi na Ufichuaji. Wahusika wanakubali kutumia Maelezo ya Faraghani ya yule mwingine ili tu kutekeleza majukumu husika hapa, na hatafichua, kupatiana, kuhamisha, kufanya kupatikana, au vinginevyo kuwasilisha Maelezo ya Faraghani ya yule mwingine kwa wahusika wengine; mradi kwamba Maelezo ya Faraghani yanaweza kufichuliwa kwa Wanakandarasi Wadogo wa Mhusika huyo ambaye ana hitaji la kujua maelezo hayo ili kutekeleza majukumu yake chini ya Makubaliano haya, na yuko chini ya majukumu ya faragha angalau kama inavyowekewa vikwazo hapa. Kila Mhusika atawajibikia ukiukaji wowote wa kauli hii na Wanakandarasi wake Wadogo. Sehemu hii ya 11(b) haitatumika kwa Maelezo ya Faraghani ambayo: (i) yalikuwa hadharani kufikia wakati yalipowasilishwa kwa mpokeaji au yaliwekwa hadharani kupitia makosa ambayo si ya Mhusika au mpokeaji anayeyafichua; (ii) mpokeaji anaweza kuthibitisha yalitengenezwa kwa njia huru na mpokeaji au tayari yalijulikana na mpokeaji kufikia wakati wa kuyapokea (bila kipimo cha majukumu yoyote yaliyo hapa); (iii) yaliwasilishwa kwa mpokeaji kwa njia sahihi, bila jukumu lolote la kutofichua au kikwazo cha matumizi; au (iv) yanahitajika kufichuliwa kulingana na amri ya mahakama au amri nyingine ya sheria, mradi iwe Mhusika anayepokea atamuarifu Mhusika yule mwingine bila kuchelewa kuhusu kigezo hicho, na ataambatana na amri ya kulinda au sawa iliyotolewa kwa ajili ya ufichuaji huo.. Endapo kuna ifichuaji bila idhini wa Maelezo ya Faraghani, Mhusika anayefichua anachukua mzigo wa kutoa ushahidi kwamba msingi mmoja au zaidi wa iliyotajwa hapa juu inatumika.

c. Maelezo ya Kibinafsi. Bila kuwekea kipimo majukumu yaliyotajwa hapo juu kwa namna yoyote, Mshirika wa Ufikishaji anaelewa na kukubali kwamba (i) maelezo yaliyojumuishwa katika sehemu ndogo za 10(a)(i) na 10(a)(ii) hapa juu na (ii) maelezo mengine yote ambayo Mshirika wa Ufikishaji anachakata kuhusiana na utoaji Huduma za Ufikishaji ambao uko chini ya sheria, masharti, na kanuni za faragha na ulinzi wa data za kimataifa, kitaifa, na jimbo kuhusiana na faragha, uchakataji na utumiaji wa data, ulinzi wa data, usalama wa data, usimbaji, au ufaragha, ikijumuisha laini si tu, sheria ya California Consumer Privacy Act, Cal. Civ. Code §§ 1798.100 et seq. (“CCPA”) ((i) na (ii) kwa pamoja, “Maelezo ya Kibinafsi”) yako chini ya vikwazo vya ziada kama ilivyobainishwa hapa chini. Kwa ajili ya Sehemu hii ya 11(c), mchakato inamaanisha operesheni yoyote au kundi la operesheni ambazo zinafanywa kwenye Maelezo ya Kibinafsi, iwe ni kwa njia za kiotomatiki au la.

i. Wahusika wanatambua na kukubali kwamba Mshirika wa Ufikishaji atatenda kama “Mtoa Huduma” na si “Mhusika Mwingine” kulingana na CCPA na kama ilivyobainishwa katika CCPA katika utekelezaji wake wa majukumu yake kulingana na Makubaliano.

ii. Mshirika wa Ufikishaji (i) hatauza (kama ilivyobainishwa kwenye CCPA) Maelezo yoyote ya Kibinafsi kwa biashara nyingine au mhusika mwingine bila idhini ya awali kwa maandishi kutoka kwa Grubhub, (ii) hatahifadhi, kutumia wala kufichua Maelezo ya Kibinafsi kwa malengo yoyote kando na malengo maalum ya kutoa Huduma za Ufikishaji, ikijumuisha kuhifadhi, kutumia, au kufichua Maelezo ya Kibinafsi kwa malengo ya kibiashara kando na kutoa Huduma za Ufikishaji au (iii) hatahifadhi, kutumia wala kufichua Maelezo ya Kibinafsi nje ya uhusiano wa moja kwa moja wa kibiashara kati ya Wahusika. Ili kufafanua, Mshirika wa Ufikishaji hatawasiliana na wateja au Wauzaji zaidi ya inavyohitajika ili kutimiza Huduma wala kupakua na/au kuhifadhi Maelezo ya Kibinafsi ambayo Mshirika wa Ufikishaji anachakata kuhusiana na utoaji Huduma za Ufikishaji kwa wateja nje ya Programu ya Driver. Mshirika wa Ufikishaji hapa anathibitisha kwamba Mshirika wa Ufikishaji anaelewa vigezo vilivyo kwenye sentensi inayotangulia na ataambatana navyo.

iii. Isipokuwa iwe inahitajika na sheria husika, mara moja baada ya ombi kwa maandishi kutoka kwa Grubhub au katika hali ya Makubaliano hata kubatilishwa Mshirika wa Ufikishaji atafuta na kuagiza kufutwa kwa nakala zingine zozote za Maelezo ya Kibinafsi yaliyochakatwa na Mshirika wa Ufikishaji au Mwanakandarasi wake Mdogo yeyote na baadaye kupatia Grubhub thibitisho kwa maandishi.

d. Umiliki. Maelezo yote ya Faraghani yatasalia kuwa mali ya kipekee ya Mhusika anayefichua. Hakuna chochote katika Makubaliano haya kitachukuliwa kumpa Mhusika haki zozote kwenye Maelezo ya Faraghani yanayofichuliwa na Mhusika yule mwingine, au sehemu yake.

e. Ukiukaji. Endapo kuna ukiukaji wa Sehemu hii ya 11, Mhusika mlalamikaji atakuwa na haki ya kudai urejeshaji mara moja wa Malezo yote ya Faraghani na kufidia hasara zote zinazoibuka kwa sababu ya ukiukaji huo kulingana na Kauli ya Usuluhishaji (kama ilivyobainishwa katika Sehemu ya 13). Wahusika haswa wanatambua kwamba matumizi au ufichuaji bila idhini wa Maelezo ya Faraghani unaweza kupelekea madhara yasiyoweza kusuluhika ambapo hakuna suluhu tosha ya kisheria, na katika tukio hilo Mhusika mlalamikaji atakuwa na haki ya kupata amri ya mchakato wa usuluhishaji, au suluhu nyingine yoyote inayopatikana katika sheria au sawa ili kuzuia matumizi au ufichuaji zaidi bila idhini, na kwamba hakuna dhamana itahitajika. Kukosa kuambatana na sehemu yoyote ya Sehemu ya 11 ni ukiukaji mkubwa wa Makubaliano haya.

12. Kipindi; Ubatilishaji.

a. Ubatilishaji. Makubaliano haya yataanza tarehe ambayo Makubaliano haya yanatiwa sahihi ("Tarehe ya Kuanza Kutumika"), na kuendelea mpaka yatakapobatilishwa na Mhusika mmoja kulingana na Sehemu ya 2(d), Sehemu ya 4(a) au Sehemu hii ya 12.

i. Ukiukaji Mkubwa. Mhusika mmoja anaweza kubatilisha Makubaliano haya mara moja endapo Mhusika huyo mwingine atakiuka kauli yoyote ya Makubaliano haya kwa kumpa Mhusika huyo mwingine ilani kwa maandishi na kutambulisha ukiukaji husika. Mifano ya ukiukaji mkubwa na Mshirika wa Ufikishaji inajumuisha, lakini si tu, yafuatayo:

1. Ukiukaji wowote wa Sehemu ya 2(d) au 4(a) ya Makubaliano haya;

2. Ukiukaji wowote wa sheria au kanuni husika kuhusiana na utekelezaji Huduma za Ufikishaji, iwe ukiukaji huo ulipelekea hatua ya kisheria au la;

3. Hatua yoyote inayoathiri vibaya sifa za Grubhub au uhusiano wake na Wauzaji au wateja wanaotumia Mfumo (ikijumuisha tabia katili, chafu, ya utelekezaji au vinginevyo isiyo ya kitaalamu huku akitekeleza Huduma za Ufikishaji);

4. Hatua yoyote ambayo ni ya kiulaghai, danganyifu; au inadakiza pakubwa uendeshaji biashara ya Grubhub;

5. Hatua yoyote inayotishia usalama wa Mshirika wa Ufikishaji au Mwanakandarasi Mdogo, au mfanyikazi wa Muuzaji, mteja au mfanyikazi wa Grubhub (ikijumuisha bila kipimo, kuendesha gari au pikipiki kiholela, matisho na ukali, kufuatilia kwa siri na/au kuwasiliana na watu bila idhini);

6. Kuwa mlevi wa bidhaa haramu au pombe huku ukitekeleza Huduma za Ufikishaji; au

7. Ukiukaji wowote mkubwa wa au sababu zilizobainishwa katika **Sheria za Matumizi za Mshirika wa Ufikishaji wa Grubhub**, **Sera ya Faragha ya Mshirika wa Ufikishaji wa Grubhub**, **Sheria za Matumizi za Grubhub**, na sera na miongozo mingine yoyote husika.

ii. Kwa Kurahisishia Mshirika wa Ufikishaji. Mshirika wa Ufikishaji ana haki ya kubatilisha Makubaliano kwa sababu yoyote baada ya ilani kwa maandishi ya siku 30.

iii. Afya na Usalama wa Umma; Mazingatio ya Kishughuli. Grubhub inaweza kusimamisha au kubatilisha makubaliano haya ya Mshirika wa Ufikishaji na uwezo wa Mshirika wa Ufikishaji wa kufikia Mfumo ikiwa Mshirika wa Ufikishaji atapatikana kuwa na hatia ya kijinai ambayo inaweza kuathiri vibaya uwezo wa Mshirika wa Ufikishaji kutekeleza Huduma za Ufikishaji au kuweka wateja wa Grubhub, umma au kundi lingine lolote la watu katika hatari isiyofaa. Historia yoyote kama hiyo ya kupatikana na hatia itakaguliwa na kutathminiwa kibinafsi kulingana na vigezo, ikiwa vipo, vya sheria husika kabla ya uamuzi wowote kufanywa kuhusiana na ushirika wako na Grubhub. Pia Grubhub inaweza kusimamisha, kusitisha au kubatilisha uwezo wa Mshirika wa Ufikishaji wa kufikia Mfumo kwa mazingatio ya operesheni, pamoja na hitaji la masoko, usitishaji kabisa au kwa sehemu tu wa Programu ya Driver au Mfumo, na mazingatio ya kiudhibiti ya ndani.

iv. Kudumu. Haki na majukumu yaliyobainishwa katika Sehemu za 5, 6, 8, 9, 10, 11, 12, 13 na 14 za Makubaliano haya yataendelea kutumika hata baada ya kusitishwa kwa Makubalinao haya na

Shughuli zozote hapa, na yataendelea kutumika na kwa mafao na kuwafunga Wahusika na wawakilishi wao wa kisheria, warithi wake, na wanapokea majukumu kutoka kwake.

v. Programu ya Driver. Bila kujali chochote ambacho ni kinyume na Makubaliano haya na bila ilani ya mapema au dhima kwa Mshirika wa Ufikishaji, Grubhub inaweza kubadilisha, kuzuia, au kusimamisha uwezo wa Mshirika wa Ufikishaji wa kufikia Programu ya Driver, kwa muda tu au au kabisa daima, ikiwa Mshirika huyo wa Ufikishaji au Mwanakandarasi huyo Mdogo anadhaniwa au kwa sababu tosha anadhaniwa kuwa amekiuka Makubaliano haya, kwa malengo ya uchunguzi ambapo ulaghai au matumizi mabaya yanadhaniwa, au wakati inahitajika ili kulinda usalama na ulinzi wa wateja, Wauzaji, na umma kwa jumla. Grubhub itampa Mshirika wa Ufikishaji fursa ya kukata rufaa kuhusu usitishaji wa uwezo wa Mshirika wa Ufikishaji wa kufikia Programu ya Driver au kikwazo dhidi ya Mshirika wa Ufikishaji kuhusiana na Programu ya Driver.

b. Mpango wa Huduma. Wahusika wanatambua kwamba kipindi cha Makubaliano haya hakionyeshi mpango wa huduma bila kudakizwa. Grubhub inaweza kuweka Ofa za Ada kwa hiari yake, na Mshirika wa Ufikishaji anaweza kukubali au kukataa Ofa za Ada kwa hiari yake. Hakuna wakati Grubhub inaweza kuhitajika kuweka idadi fulani cha Ofa za Ada kwa Mshirika wa Ufikishaji, na pia Mshirika wa Ufikishaji hatahitajika kukubali idadi fulani ya Shughuli. Hakuna Huduma za Ufikishaji zitatekeleza bila makubaliano ya pamoja ya Wahusika kuhusu Shughuli.

13. Usuluhishaji wa Pamoja. Kwa kiwango kamili kinachoruhusiwa na sheria, Wahusika wanakubaliana pamoja kusuluhisha migogoro yoyote na yote kati yao kupitia mchakato wa usuluhishaji mbele ya JAMS, badala ya mahakamani na kwa kesi yenye waamuzi au mbele ya shirika lolote la kiutawala au kiudhibiti (isipokuwa iwe imebainishwa vinginevyo hapa chini). Makubaliano haya ya usuluhishaji (“Kauli ya Usuluhishaji”) yatatumika kwenye mgogoro wowote unaohusisha Mshirika wa Ufikishaji, Mwanakandarasi yeyote Mdogo, Grubhub na/au mshirika yeyote wa Grubhub ambaye anafanyiwa Huduma za Ufikishaji na Mshirika wa Ufikishaji. Kauli ya Usuluhishaji inatawaliwa na sheria ya Federal Arbitration Act, 9 U.S.C. §§ 1- 16 (“FAA”), na itatumika kwenye madai yoyote na yote yanayoibuka kutokana au kuhusiana na Makubaliano haya (ikijumuisha kubatilishwa kwa Makubaliano haya), ainisho na hadhi ya Mshirika wa Ufikishaji kama mwanakandarasi huru kwa Grubhub au washirika wake, ombi la Mshirika wa Ufikishaji la Akaunti, utoaji Huduma za Ufikishaji hapa au kipengele kingine chochote cha uhusiano kati ya Mshirika wa Ufikishaji, Mwanakandarasi yeyote Mdogo, Grubhub na/au mshirika yeyote wa Grubhub, iwe yanaibuka chini ya sheria za kitaifa, jimbo au ndani na/au sheria ya kawaida. Mahakama ya mamlaka adilifu au msuluhishaji akikataa kutumia sheria ya FAA kwenye makubaliano haya, basi atatumia sheria inayotawala makubaliako ya usuluhishaji katika jimbo ambako Mshirika wa Ufikishaji alitekeleza Huduma za Ufikishaji mara ya mwisho kwa wateja wa Grubhub. Endapo sehemu yoyote ya Kauli hii ya Usuluhishaji itapatikana kuwa haiwezi kutekelezeka, itaondolewa kwenye Makubaliano jinsi ambavyo sehemu inayosalia ya Kauli hii ya Usuluhishaji itatekelezwa kwa kiwango kamili kinachoruhusiwa na sheria. Ni msuluhishaji pekee, na si mahakama au shirika lolote za kitaifa, jimbo, au ndani, atakuwa na mamlaka kamili ya kusuluhisha mgogoro wowote unaohusiana na tafsiri, matumizi, utekelezekaji, uondoaji au muundo wa Kauli hii ya Usuluhishaji. Hata hivyo, bila kujali sentensi iliyotangulia, migogoro yote inayohusiana au kuibuka kutokana na Uondoaji Kesi ya Pamoja na Kigezo cha Kesi ya Kibinafsi cha Sheria Jumla ya California ya Mwanasheria wa Kibinafsi hapa chini—ikijumuisha, lakini si tu, dai lolote kwamba Uondoaji Kesi ya Pamoja au Kigezo cha Kesi ya Kibinafsi cha Sheria Jumla ya California ya Mwanasheria wa Kibinafsi haziwezi kutekelezeka, hazieleweki, ni haramu, ni batili, au inaweza kubatilishwa—itaamuliwa tu na mahakama ya mamlaka adilifu na si msuluhishaji. Migogoro yote inayohusiana au kuibuka kutokana na malipo ya ada za usuluhishaji itaamuliwa tu na msuluhishaji. Makubaliano haya hayasimamii migogoro ambayo, kisheria (baada ya kutumia sheria ya FAA), haiwezi kupitia makubaliano ya kabla ya usuluhishaji. Bila kujali masharti mengine yoyote ya Makubaliano haya, hakuna kitu chochote kinamzuia Mshirika wa Ufikishaji kupiga ripoti au kuandikisha dai au kushtaki kwa Tume ya Nafasi Sawa za Ajira, Idara ya Leba ya Marekani, Tume ya Uzaaji wa Hisa, Bodi ya Mahusiano ya Leba ya Kitaifa, au Ofisi ya Kitaifa ya Mipango ya Kuambatana na Mikataba. Hakuna kitu chochote katika makubaliano haya kinazuia uchunguzi wa shirika la serikali kwenye ripoti, dai au shtaka lolote ambalo linasimamiwa na kauli hii ya usuluhishaji. Hakuna kitu chochote katika Makubaliano haya kinamzuia Mshirika wa Ufikishaji kuarifa shirika lolote la jimbo, mkuu wa mashtaka mwingine wa umma, shirika la utekelezaji sheria, au shirika lingine lolote la serikali kuhusu ukiukaji wowote wa sheria unaodaiwa.

a. Kongamano Lisilo Rasmi la Usuluhishaji Migogoro la Kabla ya Usuluhishaji. Kabla ya kuanzisha usuluhishaji binafsi na JAMS, Wahusika ni lazima wahusike katika jitihada yenye nia nzuri ya kusuluhisha dai lolote lililosimamiwa na Kauli hii ya Usuluhishaji kupitia kongamano lisilo rasmi la kusuluhisha migogoro kwa simu kati ya Mshirika wa Ufikishaji na Grubhub. Kigezo hiki cha kongamano lisilo rasmi la

kusuluhisha migogoro kwa simu kitatumika kwa Grubhub na Mshirika wa Ufikishaji. Mhusika anayeanzisha dai ni lazima atoe ilani kwa Mhusika huyo mwingine kwa maandishi kuhusu nia yake ya kuanzisha kongamano lisilo rasmi la kusuluhisha mgogoro kwa simu, ambalo litafanyika ndani ya siku saba baada ya Mhusika huyo mwingine kupokea ilani hiyo (isipokuwa muda uongezwe kwa makubaliano ya Wahusika wote wawili). Kushiriki katika kongamano lisilo rasmi la kusuluhisha mgogoro kwa simu ni sharti ambalo kwanza lazima litimizwe kabla ya kuanzisha usuluhishaji binafsi. Sheria ya vizuizi itatozwa wakati Wahusika wanashiriki katika mchakato usio rasmi wa kusuluhisha mgogoro unaohitajika na aya hii.

b. Ilani. Ni tu baada ya Wahusika kushiriki atika nia njema ya kusuluhisha mgogoro huo kupitia kongamano lisilo rasmi la kusuluhisha mgogoro kwa simu, na ni tu ikiwa juhudi hizo hazikufaili, Mhusika mmoja anaweza kuanzisha usuluhishaji kwa kumwarifu Mhusika huyo mwingine kwa maandishi kupitia barua rasmi, ameomba thibitisho la kupokea kutumwa, au ufikishaji kwa mkono ndani ya kipindi cha sheria husika za vizuizi. Dai la usuluhishaji ni lazima lijumuishe (i) jina, nambari ya simu, anwani ya barua, na anwani ya barua pepe ya mtu au mhusika anayetaka usuluhishaji (ikiwa Mshirika wa Ufikishaji anataka usuluhishaji, anwani ya barua pepe inayopatianwa ni lazima iwe anwani ya barua pepe inayohusishwa na akaunti ya Grubhub ya Mshirika wa Ufikishaji) ; (ii) maelezo ya madai ya kisheria yanayoletwa na misingi ya kweli ya madai hayo; (iii) maelezo ya suluhu inayotafutwa na hesabu sahihi na ya nia njema ya kiwango kinachojadiliwa, kwa sarafu ya Dola za Marekani; (iv) sahihi ya Mhusika binafsi anayetaka usuluhishaji; na (v) mgao wa Mhusika wa ada ya kuandikisha kwa JAMS. Ombi lolote la suluhu ya lazima au ada za wakili halitazingatiwa kwenye hesabu ya kiwango kinachojadiliwa isipokuwa iwe suluhu hiyo ya lazima inataka malipo ya pesa. Ikiwa Mhusika anayetaka usuluhishaji anawakilishwa na wakili, basi wakili huyo ni lazima aweke sahihi yake binafsi kwenye dai la usuluhishaji. Kwa kutia sahihi dai la usuluhishaji, wakili anathibitisha kwa kadri ya ufahamu wa wakili, maelezo, na imani, inayoundwa baada ya uchunguzi unaokubalika chini ya hali ambayo: (1) dai la usuluhishaji haliwasilishwi kwa madhumuni yoyote yasiyofaa, kama vile kunyanyasa, kusababisha ucheleweshaji usiofaa, au kuongeza gharama ya usuluhishaji mgogoro bila sababu; (2) madai na mizozano mingine ya kisheria inaruhusiwa na sheria iliyopo au kwa hoja isiyo na msingi ya kupanua, kurekebisha, au kutengua sheria iliyopo au kwa kuanzisha sheria mpya; na (3) mizozano ya ukweli na uharibifu yana msaada wa ushahidi au ikiwa itatambuliwa haswa, kuna uwezekano wa kupata usaidizi wa ushahidi baada ya fursa nzuri kwa uchunguzi zaidi au ugunduzi. Dai lolote la usuluhishaji linaloelekezwa kwa Grubhub ni lazima likabidhiwe ajenti rasmi wa Grubhub wa kupokea hati hizo.. Tafadhali tazama tovuti ya Waziri wa Ndani wa jimbo lako ili kujua jina na maelezo ya mawasiliano ya ajenti rasmi wa sasa wa Grubhub. Ajenti rasmi wa Grubhub atakubali kukabidhiwa tu ikiwa mhusika kwa ambaye hati imeelekezwa analingana na jina la mhusika aliyesajiliwa na Waziri wa Ndani. Dai lolote la usuluhishaji la Gribhub ni lazima lifikishwe kwenye anwani ya kibiashara inayojulikana mwisho ya Mshirika wa Ufikishaji. Sehemu hii ya 13(b) pia itajumuisha utoaji ilani kwa ilani zote hapa, isipokuwa kwamba ilani kando na za kuanzisha usuluhishaji zinaweza pia kutumwa kupitia barua pepe kwa anwani teule ya barua pepe.

c. Uondoaji Kesi ya Pamoja. Wahusika wanakubali kwamba migogoro au madai yoyote na yote kati ya Wahusika yatasuluhishwa katika usuluhishaji binafsi. Wahusika pia wanakubali kwamba kuhusiana na kuingia katika Kauli hii ya Usuluhishaji, wote wawili wanaondoa haki ya mgogoro au dai lolote lililoletwa, kusikilizwa, kuendeshwa, au kusuluhishwa kama kesi ya pamoja, jumla, na/au ya uwakilishi, na msuluhishaji hatakuwa na mamlaka yoyote ya kusikiliza au kusuluhisha kesi yoyote ya pamoja, jumla au ya uwakilishi, ikijumuisha lakini si tu, madai yaliyoletwa chini ya sheria ya jimbo lolote ya mwanasheria wa kibinafsi (kando na madai ya Sheria Jumla ya California ya Mwanasheria wa Kibinafsi jimboni California, ambayo yameangaziwa hapa chini) ("Uondoaji Kesi ya Pamoja"). Uondoaji huu wa Kesi ya Pamoja hauzuii Wahusika kushiriki katika usuluhishaji wa pamoja wa madai. Katika tukio lolote ambapo (i) mgogoro unaandikishwa kama kesi ya pamoja, jumla, na/au ya uwakilishi na (ii) na kuna uamuzi wa mwisho wa mahakama kwamba sehemu ya Uondoaji Kesi ya Pamoja au yote haiwezi kutekelezwa, basi kesi hiyo ya pamoja, jumla, na/au uwakilishi ni lazima ifanyike katika mahakama ya umma yenye mamlaka adilifu, lakini kwa kiwango ambacho Uondoaji Kesi ya Pamoja unaonekana hauwezi kutekelezeka, na sehemu ya Uondoaji Kesi ya Pamoja ambayo inaweza kutekelezeka itatekelezwa katika usuluhishaji.

d. Kigezo cha Kesi ya Kibinafsi cha Sheria Jumla ya California ya Mwanasheria wa Kibinafsi (California Private Attorneys General Act ("PAGA") Individual Action Requirement). Wewe na Grubhub mnakubali kusuluhisha madai ya PAGA kwa misingi ya kibinafsi pekee. Hivyo basi, dai lolote lako nchini ya PAGA la kupata mishahara ambayo haijalipwa, adhabu za umma, au fidia zingine za kibinafsi ni lazima lisuluhishwe chini ya Makubaliano haya. Wewe na Grubhub pia mnakubali na kueleza kwamba madai yoyote ya PAGA yasiyo ya kibinafsi yatasalia kwenye mahakama ya kesi, na kusubiri uamuzi wa mwisho

na kwa kwa maandishi wa Msuluhishaji katika usuluhishaji kuhusiana na hali Yako inayodaiwa kama "mwajiriwa" na hali yako ya kuwa "mlalamikaji," na Wewe pamoja na Kampuni mnakubali kwamba Msuluhishaji, na si mahakama, atafanya uamuzi huu. Kifungu hiki cha Kigezo cha Kesi ya Kibinafsi cha PAGA kitaondolewa kwenye Makubaliano haya ikiwa kuna uamuzi wa mwisho wa mahakama kwamba si halali, hakiwezi kutekelezeka, hakieleweki, ni batili au kinaweza kubatilishwa. Katika tukio hilo, kesi ya PAGA ni lazima ifanyike katika mahakama ya umma ya mamlaka adilifu—si katika usuluhishaji—lakini sehemu yoyote ya Kigezo cha Kesi ya Kibinafsi cha PAGA ambayo inaweza kutekelezeka itatekelezwa katika usuluhishaji.

e. <u>Utaratibu</u>. Usuluhishaji wowote utatawaliwa na Sheria na Taratibu za Kina za Usuluhishaji za JAMS ("Sheria za JAMS"), zinazoweza kupatikana kwenye www.jamsadr.org au kwa ombi kutoka kwa Grubhub, isipokuwa kama ifuatavyo:

i. Wahusika watahitajika kukutana na kukubaliana kuchagua msuluhishaji asiyependelea upande wowote miongoni kwa wateule wa JAMS. Ikiwa wahusika hawawezi kukubaliana pamoja kuhusu msuluhishaji, basi usuluhishaji utasikilizwa na msuluhishaji mmoja aliyechaguliwa kulingana na Sheria za JAMS. Msuluhishaji atakuwa wakili au jaji mstaafu mwenye uzoefu katika sheria zinazohusu mgogoro huo.

ii. Ikiwa Wahusika hawawezi kukubaliana kuhusu eneo la usuluhishaji huo, usuluhishaji utafanyika katika kaunti ambayo Mshirika wa Ufikishaji alitekeleza Huduma za Ufikishaji chini ya Makubaliano haya.

iii. Isipokuwa sheria husika ibainishe vinginevyo, kama ilivyobainishwa na msuluhishaji, Grubhub na Mshirika wa Ufikishaji pamoja watagawana kwa usawa ada za kuandikisha na gharama zingine sawa na za kawaida za ofisi, kama ilivyo kawaida na kesi za mahakamani na kiutawala. Grubhub italipa gharama zozote zinazohusishwa kwa njia ya kipekee na usuluhishaji, kama vile ada na gharama za msuluhishaji.

iv. Mhusika akiwasilisha ofa ya uamuzi chini ya sheria ya Federal Rule of Civil Procedure 68, au nyingine sawa ya jimbo, na uamuzi ambao Mhusika huyo anapata mwishowe si mzuri zaidi kuliko ofa iliyokataliwa, basi Mhusika huyo mwingine atalipia gharama, pamoja na ada za kuandikisha, zilizotokeoa baada ya ofa kulipwa.

v. Msuluhishaji anaweza kutoa amri (ikijumuisha amri kwa wahusika wengine) na kuwezesha wahusika kutekeleza ufichuaji tosha ili kuwezesha kila Mhusika kujiandaa madai na/au utetezi wa Mhusika huyo, na kuzingatia kwamba usuluhishaji umepangwa kuwa mbinu ya haraka na fanisi ya kusukuhisha migogoro.

vi. Isipokuwa kama ilivyobainishwa katika Uondoaji Kesi ya Pamoja na Kigezo cha Kesi ya Kibinafsi cha PAGA, msuluhishaji anaweza kutoa suluhu zote ambazo mhusika katika usuluhishaji anastahili kupata chini ya sheria husika na ambazo zinaweza kupatikana mahakamani, lakini hatakuwa na mamlaka ya kupatiana suluhu zozote ambazo haziwezi kupatikana mahakamani kwa madai yaliyowasilishwa kwenye usuluhishaji. Msuluhishaji atatumia sheria husika za jimbo au kitaifa, au zote mbili, inavyohusika. Suluhu hizo zinajumuisha, lakini si tu, vikwazo vinavyopatikana chini ya sheria ya Federal Rule of Civil Procedure 11.

vii. Tokeo lolote kwamba dai au dai la kupinga liliandikishwa kwa malengo ya unyanyasaji basi Mhusika huyo mwingine atakuwa na haki ya kufidiwa ada zake za wakili na gharama zake.

viii. Msuluhishaji anaweza kusikiliza maombi ya kutupilia mbali na/au maombi ya maamuzi ya mwisho. Msuluhishaji hawezi kuruhusu kuandikishwa kwa maombi ya maamuzi ya mwisho mpaka baada ya wahusika kutekeleza uvumbuzi ili kuunga mkono madai na tetezi zao, na baada ya vigezo vya awali vya kuandikisha kesi za mahojiano chini ya sheria za JAMS kutimizwa. Maombi yyote ya kutupilia mbali na/au maombi ya maamuzi ya mwisho yatatawaliwa na viwango vya sheria za Federal Rules of Civil Procedures zinazotawala maombi hayo.

ix. Uamuzi au suluhu ya msuluhishaji itakuwa kwa maandishi na kujumuisha ushahidi wa kweli na ufafanuzi wa sheria.

i. Msuluhishaji hajafungwa na maamuzi yanayoafikianwa katika michakato tofauti ya usuluhishaji, na uamuzi wa msuluhishaji utakuwa wa kufunga tu wahusika katika usuluhishaji ambao wapo chini ya

maamuzi hayo.

xi. Wahusika wanaweza kutuma ombi kwa mahakama ya mamlaka adilifu kupata suluhu ya lazima ya muda tu au ya mapema ili kudumisha hali iliyopo au kuzuia uwezekano wa madhara yasiyoweza kurekebishika huku wakisubiri suluhu ya mwisho ya kesi ya usuluhishaji. Endapo wakati wowote msuluhishaji au msimamizi wa usuluhishaji anakosa kutekeleza masharti ya Makubaliano haya, Mhusika mmoja anaweza kuomba kushikanisha kesi ya usuluhishaji katika mahakama ya mamlaka adilifu, na usuluhishaji utasimama kiotomatiki na kusubiri tokeo la kesi hiyo.

f. Usuluhishaji wa Wingi. Endapo kuna zaidi ya madai 25 ya usuluhishaji ambayo yanafanana pakubwa yaliyoandikishwa kwenye JAMS dhidi ya Grubhub na kampuni moja ya mawakili au mkusanyiko wa kampuni za mawakili ndani ya siku 180 za kila moja, basi Taratibu na Miongozo ya Usuluhishaji kwa Wingi ya JAMS (JAMS Mass Arbitration Procedures and Guidelines) zitatumika, ambazo zitapatikana kwenye www.jamsadr.com/mass-arbitration-procedures.

g. Haki ya Kujiondoa. Kila Mshirika wa Ufikishaji ana haki ya kujiondoa kwenye Kauli hii ya Usuluhishaji kwa kutuma ilani ya barua pepe kwa anwani driverinfo@grubhub.com na kutaja nia hiyo ya kujiondoa. Mshirika wa Ufikishaji pia anaweza kuiondoa kwa kutuma ilani kwa maandishi kwa anwani Grubhub at 222 W Merchandise Mart Plaza, 8th Floor, Chicago, IL 60654, Attn: General Counsel, au kwa anwani nyingine inayobainishwa na Grubhub. Ikiwa Wewe ni Mshirika wa Ufikishaji ambaye upo tayari na umekubaliana na toleo la mbeleni la Makubaliano haya bila kujiondoa kwenye kauli ya Usuluhishaji iliyo hapo ndani, unaweza kutumia haki yako ya kujiondoa kwenye Kauli hii ya Usuluhishaji. Hata hivyo, katika tukio hilo, wewe kukubali Makubaliano haya au wewe kujiondoa kwenye Kauli hii ya Usuluhishaji hakutaathiri uhalali au uwezo wa kutekelezeka wa Kauli yoyote kama hiyo ya Usuluhishaji, na utasalia kufungwa na Kauli ya Usuluhishaji ambayo ilikufunga wakati ulipopokea Makubaliano haya. Ili iweze kutumika, ilani yoyote ya kujiondoa ni lazima iwe ya ndani ya siku 30 tangu Mshirika wa Ufikishaji akubali Makubaliano haya. Mshirika wa Ufikishaji akijiondoa kama ilivyobainishwa katika Sehemu hii ya 13(g), hautakumbwa na madhara yoyote mabaya kutokana na uamuzi huo na unaweza kutafuta suluhu za kisheria bila kuhusisha Kauli hii ya Usuluhishaji. Mshirika wa Ufikishaji akikosa kujiondoa kwenye Kauli hii ya Usuluhishaji ndani ya siku 30 tangu Mshirika wa Ufikishaji akubali Makubaliano haya, kukubali huko kwa Makubaliano haya kutamaanisha Grubhub na Mshirika wa Ufikishaji kwa pamoja wanakubali masharti ya Kauli hii ya Usuluhishaji.

h. Haki ya Kushauriana na Wakili. Mshirika wa Ufikishaji anatambua kwamba amepewa fursa ya kushauriana na wakili wa kibinafsi kuhusu chaguo lake kuhusiana na kama atakubaliana na kipengele chochote na dai lolote ambalo linaweza kuwa chini ya Kauli hii ya Usuluhishaji. Isipokuwa kama ilivyoelezewa katika sehemu ndogo ya (c) hapa juu, endapo sehemu yoyote ya Kauli hii ya Usuluhishaji itapatikana kuwa haiwezi kutekelezeka, sehemu inayosalia ya Kauli hii ya Usuluhishaji itatekelezwa.

i. Athari kwenye Kesi Inayoendelea. Kauli hii ya Usuluhishaji haitaathiri msimamo wa Mshirika wa Ufikishaji kuhusiana na kesi yoyote dhidi ya Grubhub iliyoletwa na Mshirika wa Ufikishaji au kwa niaba ya Mshirika wa Ufikishaji inayoendelea katika mahakama ya jimbo au kitaifa au usuluhishaji kufikia tarehe ya Mshirika wa Ufikishaji kupokea Kauli hii ya Usuluhishaji ("Kesi Inayoendelea"). Hivyo basi, ikiwa Mshirika wa Ufikishaji ameidhinishwa au hapo awali alikuwa ameidhinisjwa kutumia Mfumo wa Grubhub na Programu ya Driver, na wakati wa Mshirika wa Ufikishaji kupokea makubaliano haya Mshirika wa Ufikishaji hakufungwa na Kauli iliyopo ya Usuluhishaji ya pamoja na Grubhub, Mshirika wa Ufikishaji atasalia kustahiki kushiriki katika Kesi yoyote Inayoendelea kwa ambayo Mshirika wa Ufikishaji alikuwa mhusika au mhusika katika kesi ya pamoja, jumla, au ya uwakilishi bila kujali kama Mshirika wa Ufikishaji anajiondoa kwenye Kauli hii ya Usuluhishaji. Ikiwa, wakati wa Mshirika wa Ufikishaji kupokea makubaliano haya, Mshirika wa Ufikishaji alifungwa na Kauli iliyopo ya Usuluhishaji ya pamoja na Grubhub, Kauli hiyo ya Usuluhishaji itaendelea kutumika kwenye Kesi yoyote Inayoendelea, hata kama Mshirika wa Ufikishaji anajiondoa kwenye Kauli hii ya Usuluhishaji. Ikiwa, wakati wa Mshirika wa Ufikishaji kupokea makubaliano haya, Mshirika wa Ufikishaji hapo awali hakuwa ameidhinishwa kutumia Mfumo wa Grubhub na Programu ya Driver, basi Kauli hii ya Usuluhishaji itatumika kwenye madai yote na Kesi yoyote Inayoendelea isipokuwa Mshirika wa Ufikishaji ajiondoe kwenye Kauli hii ya Usuluhishaji kama ilivyobainishwa hapa juu.

14. UONDOAJI HAKI YA KESI YA PAMOJA

Kwa kiwango kinachoruhusiwa na sheria husika, tofauti na kando na Kauli ya Usuluhishaji wa Pamoja katika sehemu ya 13, inavyohusika, Mshirika wa Ufikishaji na Grubhub wanakubali kwamba kesi zozote

mahakamani kuhusu mgogoro wowote unaoibuka au kutokana na Makubaliano haya, iwe ni kwa sababu Mshirika wa Ufikishaji alijiondoa kwenye Kauli ya Usuluhisjai wa Pamoja au kwa sababu nyingine yoyote, itafafanywa kwenye misingi ya kibinafsi, na wahusika wanakubali kutokuwa na hali yoyote tatanishi, dai lolote au mgogoro wowote kusikilizwa kama kesi ya pamoja, uwakilishi, au ya jumla, jumla ya mwanasheria wa kibinafsi, au katika kesi yoyote ambayo Mshirika wa Ufikishaji au Grubhub inatenda au kupendekeza kutenda kama mwakilishi ("Uondoaji Haki ya Kesi ya Pamoja"). Mshirika wa Ufikishaji na Grubhub pia wanakubali kwamba hakuna kesi itashikanishwa, kujumuishwa, au kuchanganywa na kesi nyingine, bila idhini ya mapema kwa maandishi ya wahusika wote kuhusu kesi yoyote kama hiyo. Ikiwa mahakama yenye mamlaka thabiti itaamua kwamba sehemu yoyote au zote za Uondoaji Haki ya Kesi ya Pamoja haziwezi kutekelezeka, haziwezi kueleweka, ni batili au zinaweza kubatilishwa, sehemu inayosalia ya Makubaliano haya itaendelea kutumika kikamilifu. Ili kufafanua, hakuna kitu chochote katika sehemu hii kitachukuliwa kupinga suluhu kwa misingi ya pamoja, jumla, na/au uwakilishi.

15. Marekebisho

   a. Isipokuwa Kauli ya Usuluhishaji wa Pamoja katika Sehemu ya 13, Grubhub inaweza kurekebisha Makubaliano haya wakati wowote. Wakati Grubhub inapofanya mabadiliko makubwa kwenye Makubaliano haya ("Makubaliano Yaliyorekebishwa"), itachapisha Makubaliano Yaliyorekebishwa kwenye Mfumo wa Grubhub, na pale inaporuhusiwa na sheria, kusambaza mapema nakala za Makubaliano hayo Yaliyorekebishwa. Utafungwa tu na Makubaliano Yaliyorekebishwa, baada ya kukubali, lakini ukikosa kuyakubali, hautaweza kufikia Mfumo etu. Vivyo hivyo, utapewa ilani kuhusu mabadiliko yoyote kwenye Kauli ya Usuluhishaji wa Pamoja, na utafungwa tu na mabadiliko hayo kwenye Kauli ya Usuluhishaji wa Pamoja baada ya kuyakubali. Hata hivyo, ukikosa kukubali yoyote ya mabadiliko hayo, hautaweza kufikia Mfumo wetu. Mabadiliko au nyongeza hizo zinaweza kutumwa kwako kupitia njia za kielektroniki. Grubhub inaweza kurekebisha **Sheria za Matumizi za Mshirika wa Ufikishaji wa Grubhub**, **Sera ya Faragha ya Mshirika wa Ufikishaji wa Grubhub**, **Sheria za Matumizi za Grubhub**, pamoja na sera na miongozo mingine yoyote wakati wowote, na marekebisho hayo yataanza kutumika yanapochapishwa.

16. Mambo Mengine.

   a. Upeanaji. Mshirika wa Ufikishaji hawezi kupeana Makubaliano haya bila idhini ya mapema ya Grubhub kwa maandishi. Chini ya haya, Makubaliano haya yatafunga na kuwa ya manufaa kwa kila warithi na wapokezi wake wa majukumu wanaoruhusiwa.

   b. Kuondolewa. Ikiwa kauli yoyote ya Makubaliano haya ni inapatikana kuwa haiwezi kutekelezeka au si ya kisheria, kauli hiyo itabadilishwa na kutafsiriwa ili kufanikisha malengo ya kauli hiyo kwa kiwango kikubwa zaidi inavyowezekana chini ya sheria husika, na kauli zinazosalia za Makubaliano haya zitaendelea kutekelezwa kikamilifu.

   c. Uondoaji Haki. Mhusika yeyote akishindwa kutekeleza kauli yoyote ya Makubaliano haya hakutachukuliwa kuwa uondoaji haki, au sababu ya Mhusika huyo mwingine kutotekeleza katika siku zijazo.

   d. Vichwa. Vichwa vinavyotokea kwenye Makubaliano haya ni ili kukurahisishia mambo na hakuna vile vinaweka vikwazo, kusisitiza, kurekebisha au vinginevyo kuathiri masharti na kauli za Makubaliano haya.

   e. Makubaliano Yote Kamili. Makubaliano haya, pamoja na viambatisho vyovyote vilivyoambatishwa hapa na makubaliano na sera nyingine zozote zinazojumuishwa kwa marejeleo hapa, yanabainisha kauli msingi zinazotawala Grubhub katika kumhusisha Mshirika wa Ufikishaji katika utoaji Huduma za Ufikishaji, na yanapiku makubaliano yoyote na yote ya hapo awali kati ya Wahusika, iwe ni kwa maandishi au matamshi. Pamoja na masharti ya Shughuli zozote zilizokubalianwa kati ya Wahusika, Makubaliano haya ni Makubaliano yote kamili kati ya Wahusika kuhusiana na mada inayojadiliwa hapa. Kwa kiwango ambapo kuna ukinzani kati ya makubaliano haya na makubaliano mengine yoyote kati ya Wahusika kuhusiana na mada inayojadiliwa na Makubaliano haya, Makubaliano haya yatatumika.

MSHIRIKA WA UFIKISHAJI ANATAMBUA, KUWAKILISHA NA KUTOA HAKIKIHO KWAMBA ANA HAKI, MAMLAKA NA UWEZO WA KUINGIA KATIKA MAKUBALIANO HAYA YA KATI YA WAHUSIKA, AMESOMA NA KUELEWA KIKAMILIFU KAULI ZA MAKUBALIANO HAYA NA AMEKUWA NA MUDA WA KUTOSHA NA FURSA TOSHA ZA KUSHAURIANA NA WASHAURI WAKE WA KIBINAFSI WA KIFEDHA, USHURU NA KISHERIA KABLA YA KUKUBALI MAKUBALIANO HAYA.

Kwa kutia alama kwenye kisanduku hiki, ninathibitisha kwamba nimesoma na kukubali kufungwa na Makubaliano haya ya Mshirika wa Ufikishaji, na kwa masharti yote yaliyo hapa ndani, na Makubaliano

haya ya Mshirika wa Ufikishaji yataanza kutumika kati ya Wahusika kuanzia tarehe ninayoweka alama kwenye kisanduku hiki ("Tarehe ya Kuanza Kutumika").